**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

# TANGAZO

## KUFUNGULIWA KWA UVUVI WA KAMBAMITI KWA MSIMU WA MWAKA, 2025

---

*(Chini ya Kifungu cha 4(3) cha Sheria ya Uvuvi, Sura 279)*

---

1. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi inalo jukumu la kisheria la kusimamia, kulinda, na kuendeleza rasilimali za uvuvi nchini na kuhakikisha rasilimali hizi zinanufaisha jamii na Taifa kwa ujumla. Ili kufanikisha malengo yanayokusudiwa Wizara ina wajibu wa kusimamia utekelezaji wa Sheria na Kanuni za Uvuvi zilizopo na kutoa miongozo mbalimbali ya kusimamia uvuvi endelevu wa samaki aina ya Kambamiti kwa lengo mahususi kudhibiti upotevu na upungufu wa rasilimali hizi muhimu za uvuvi.

2. Kama mnavyofahamu uvuvi wa samaki aina ya Kambamiti hufanyika nchini katika kanda ya Kaskazini na Kusini. Kwa kuzingatia majukumu niliyokasimishwa kwa mujibu wa sheria naelekeza Kwa msimu wa mwaka 2025 maombi ya leseni na uvuvi huu na msimu wa uvuvi utafanyika kama ifuatavyo:-

   i. Kanda ya kaskazini inahusisha maeneo ya Dar es Salaam, Tanga, Bagamoyo – Saadani. Kwa kanda hii uvuvi utafanyika kuanzia tarehe 1 Machi hadi tarehe 30 Septemba, 2025

   ii. Kanda ya kusini inahusisha maeneo ya Kisiju, Rufiji - delta, Jaja/Kilwa, Lindi na Mtwara. kwa kanda hii uvuvi utafanyika kuanzia tarehe 1 Aprili hadi 31 Agosti, 2025

   iii. Maombi ya leseni za uvuvi wa Kambamiti unaofanywa na wavuvi wakubwa, maombi yatumwe kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

   iv. Maombi ya leseni za uvuvi wa Kambamiti unaofanywa na wavuvi wadogo maombi yatumwe Halmashauri kulingana na eneo ambalo muombaji atafanya uvuvi. Maombi hayo yatumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri husika.

3. Kwa tangazo hili naelekeza kila kampuni au mwananchi mwenye nia ya kufanya uvuvi wa Kambamiti kwa msimu wa mwaka 2025 atume maombi ndani ya **siku saba (7)** kuanzia tarehe ya tangazo hili. Aidha, waombaji wanapaswa kuzingatia Sheria ya Uvuvi [Sura 279] ,Kanuni ya Uvuvi za Mwaka 2009 na marekebisho yake ya mwaka 2020. Kwa maelezo zaidi waombaji wanaombwa kutembelea Ofisi za Wizara Kanda ya Dar es Salaam na Pwani na tovuti ya wizara (*www.mifugo.uvuvi.go.tz*)

4. Tangazo hili limetolewa kwa mujibu wa Sheria. hivyo, ukiukwaji wa waraka huu ni kosa na hatua kisheria zitachukuliwa.

Prof. Mohammed A. Sheikh
**MKURUGENZI WA UVUVI**

**TARATIBU ZA KUZINGATIA KWA UVUVI WA KAMBAMITI KWA MSIMU WA MWAKA 2025.**

Uvuvi wa Kambamiti kwa msimu wa mwaka 2025 utafanyika kwa kuzingatia Sheria ya Uvuvi Namba 22 ya mwaka 2003, Kanuni za Uvuvi za mwaka 2009 na maboresho yake ya mwaka 2020 pamoja na taratibu zingine ambazo zimeandaliwa na Wizara. Taratibu hizo ni kama zifuatazo:

i. Uvuvi wa Kambamiti utafunguliwa tarehe 1 Machi mpaka tarehe 30 Septemba kwa Kanda ya Kaskazini na tarehe 1 Aprili mpaka tarehe 31 Agosti kwa Kanda ya Kusini kila mwaka kwa wavuvi wote wakubwa na wadogo.

ii. Kila muombaji atapaswa kujaza kikamilifu fomu (2a, 3a na 3b) wakati wa maombi kwa kuzingatia Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 na Kanuni zake za Mwaka 2009 na Marekebisho yake ya mwaka 2020

iii. Maombi ya leseni za uvuvi wa Kambamiti kwa wavuvi wakubwa yatumwe kwa Katibu Mkuu (Wizara ya Mifugo na Uvuvi) na wavuvi wadogo watume maombi katika Halmashauri husika.

iv. Kila chombo kitapata haki sawa. Aidha, utaratibu utakaotumika kuhusu chombo gani kinaanza mwezi Machi na chombo gani kitaendelea mpaka mwezi Septemba utapangwa na wadau watajulishwa.

v. Kila Kampuni ya Meli iliyopata kibali cha kuomba leseni itapaswa kuwasilisha 'Bank Statement' inayoonyesha uhai wa biashara husika.

vi. Makampuni yanashauriwa kuwekeza katika viwanda vya kuchakata mazao ya Uvuvi, viwanda vya kutengeneza barafu kwa ajili ya kuhakikisha ubora wa mazao ya uvuvi. Aidha, kwa wale ambao watakuwa wameshindwa kuwekeza katika viwanda, wanashauriwa kuwasilisha mikataba ambayo wameingia na wenye viwanda kwa ajili ya kuhifadhia na kuchakata mazao ya uvuvi ili kuhakikisha ubora wa mazao unazingatiwa.

vii. Kwa Makampuni yatakayoajiri wageni, yanapaswa kuwasilisha vibali vya kufanya kazi nchini kwa watu wasio raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

viii. Idadi ya meli kwa wavuvi wakubwa zitakuwa kumi na mbili (12) ambapo kila kanda zitaruhusiwa meli nne tu ambapo kutakuwa na mzunguko kwa kanda kila mwezi**.**

ix. Vyombo vitakavyotumika kwenye Uvuvi wa Kambamiti vitatakiwa kuwa na injini zisizozidi jumla ya nguvu ya Farasi 500 (500HP) na urefu kati ya mita 11.00 hadi mita 25.0, uzito usiopungua tani 20 na usiozidi tani 150 (GRT).

x. Meli ya uvuvi hairuhusiwi kutumia mnyororo wa kutifua tifua chini (tickler chain) katika Uvuvi wa Kambamiti.

xi. Wavu uwekewe kifaa kisichokamata viumbe adimu kama vile Kasa (Turtle Exclusive Device-TED) na kupunguza samaki wasiolengwa (Bycatch Reducing Device-BRD).

xii. Meli inayokokota wavu nyuma (stern) iwe na wavu mmoja na meli inayokokota wavu ubavuni (outtriggers) iwe na nyavu mbili (moja kila upande).

xiii. Chombo cha uvuvi ni lazima kiwe na kifaa kitakachoonyesha mwenendo wa meli ya Uvuvi Baharini (VMS). Gharama za kuweka kifaa cha VMS kwenye meli iwe ni ya mwenye chombo. Aidha, VMs inapaswa kuwashwa muda wote wa chombo kiwapo baharini.

xiv. Muda wa kuvua kwa meli utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili asubuhi mpaka saa kumi na mbili jioni.

xv. Eneo la Uvuvi kwa meli zisivue chini ya kina cha mita 6 kulingana na mkataba wa RAMSAR.

xvi. Chombo kitakachovua kiwe na 'Fishing Authorization Certificate' kutoka nchi ambayo meli hiyo ilikuwa inavua kwa mara ya mwisho.

xvii. Chombo kiwe na usajili kutoka TASAC na kupewa Sea Worthiness Certificate.

xviii. Chombo kitakachoomba kuvua kitakaguliwa kama hakijahusika kwenye Uvuvi haramu.

xix. Takwimu zitakazowasilishwa wakati wa kushusha mzigo zitathibitishwa na nahodha wa chombo na ''Observer wa Idara'' kwa kusainiwa na wote.

xx. Utoaji wa leseni utazingatia ''Kampuni moja meli moja'' ili kuhakikisha kuwa kila kampuni inamilikiwa na mmiliki tofauti.

xxi. Ikiwa itabainika kwamba ''Observer'', Nahodha na ''Chief Officer'' wameshiriki katika kutorosha mzigo au kutoa taarifa zisizo sahihi hatua kali za kisheria zitachukuliwa.

xxii. Idara ya Uvuvi itatoa kibali kwa meli kushusha samaki (bycatch) Bandarini au baharini. Aidha, chombo chochote hakiruhusiwi kumwaga samaki majini.

xxiii. Chombo chochote hakiruhusiwi kuchafua mazingira kama vile kutupa takataka ngumu (Plastics), Mafuta na uchafuzi mwingine unaofanana na huo.

xxiv. Meli zitakapokuwa zinavua kwenye kanda husika zifanye mawasiliano na Serikali ya Kijiji/Mtaa, mara watakapofika kwenye eneo lao na watoe taarifa wakati wanaondoka na kulipa ushuru stahiki.